# KISWAHILI LUGHA

# DARASA LA SITA

# **2015**

**AVAILABLE ONLINE AT:**

Schools Net Kenya Consultancy

**P.O. Box 8076 – 00200 Nairobi, Kenya | Tel: +254202319748**

**E-mail: infosnkenya@gmail.com | www.schoolsnetkenya.com**

**KISWAHILI**
**SEHEMU YA KWANZA:**
**LUGHA**

**Muda: Saa 1 dakika 40**

***Soma kifungu kifuatavyo. Kina nafasi 1 - 15. Katika kila nafasi, umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale manne uliyopewa***

Juzijuzi ___1___ mtaa wa Maporomoko ulio ___2___ mtaa ___3___ Hekima, kulizuka ___4___. Mzee ___5___ tamaa alitaka ___6___ mke wa tatu. Mke mwenyewe alikuwa msichana ___7___ wa darasa ___8___ tano. Fununu ___9___ majirani, walikwenda ___10___ hadi kwa chifu. Mzee Tamaa alipokamatwa na kuhojiwa, alishangaa na kusema "mimi nilishapatana na wazazi ___11___. Nimeshalipa mahari yote. Shida yote hii ___12___ wapi? Huyu ni mke ___13___ sasa."


Chifu ambaye alishangazwa na kiburi cha mzee Tamaa alitoa amri kuwa mzee huyo ___14___ mahakamani ___15___ na babake msichana ili wajibu mashtaka ya kukiuka haki za watoto.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. kuliko | B. katika | C. huku | D. huko |
| **2.** | A. ndani ya | B. karibu na | C. kwenye | D. katika |
| **3.** | A. ya | B. na | C. pa | D. kwa |
| **4.** | A. kizaazaa | B. kisasa | C. kizazi | D. kisasi |
| **5.** | A. kwenye | B. mwenye | C. mwenyewe | D. kwenyewe |
| **6.** | A. kuoleka | B. kuoa | C. kuoana | D. kuolewa |
| **7.** | A. mdogo | B. ndogo | C. kidogo | D. udogo |
| **8.** | A. ya | B. cha | C. wa | D. la |
| **9.** | A. ulipowafikia | B. ilipowafikia | C. ilipofikia | D. ilipofika |
| **10.** | A. mmoja | B. mojamoja | C. moja kwa moja | D. mmoja |
| **11.** | A. yake | B. wake | C. zao | D. yao |
| **12.** | A. imetoka | B. kimetoka | C. limetoka | D. yametoka |
| **13.** | A. yangu | B. yetu | C. wetu | D. wangu |
| **14.** | A. ifikishwe | B. lifikishwe | C. afikishwe | D. yafikishwe |
| **15.** | A. pamoja | B. wamoja | C. mmoja | D. kumoja |

***Kutoka swali la 16 - 30, jibu kulingana na maagizo.***

**16.** Kamilisha kwa kiunganishi bora.
_______ umepona, sasa tutasafiri.
A. Mighairi B. Na
C. Lakini D. Maadamu

**17.** Taja jina la umbo hili __________.



A. pembe mraba
B. pembe kali
C. pembe kuu
D. pembe butu kali

***Chagua kundi sahihi la majina halisi ya kisarufi yaliyopigiwa mstari katika mpangilio huu wa sentensi:***

Mtoto <u>yule</u> aliyeanguka vibaya ni <u>wangu</u> <u>mimi</u>

**18.** A. Kivumishi, kimilikishi, kielezi, jina
B. Kiashiria, kielezi, kimilikishi, nafsi
C. Kielezi, kivumishi, kirejeshi, kiima
D. Kitenzi, kiulizi, kiunganishi, kihusishi

**19.** Mfupa unaofunika ubongo huitwa
A. fuvu B. mtulinga
C. nguyu D. muundi

**20.** Teua jibu lisilo na mwendelezo mwafaka wa kisarufi
A. Mitego mingi mingineyo
B. Shinda nyingi, nyinginezo
C. Mifugo mingi mingineyo
D. Giza jingi jinginelo

**21.** Kengele ndogo ndogo zinazofungwa miguuni wakati wa kucheza ngoma ni
A. tari B. njuga
C. firimbi D. parapanda

**22.** Kamilisha methali: Amadi kibindoni, silaha iliyo __________.
A. tayari B.nzuri
C. karibu D. mkononi

**23.** Anayeongea kwa kudodosa au kusitasita ni kigugumizi. Anayeongea kwa ncha ya ulimi ni
A. kithembe B. kiduko
C. kibyongo D. kibunye

**24.** Kinegwe, kipusi, kifaranga, kisui wote ni
A. vimelea B. wanyama
C. vikembe D. vizazi

**25.** Mbuzi ni mnyama na pia ni kifaa cha kutumia nazi. Hii ni fani gani ya lugha
A. kisawe
B. kitate
C. istiara
D. kitawe

**26.** Chombo mfano wa gari la chuma ambacho hutumika kwa vita ni
A. nyambizi
B. kifaru
C. parange
D. kombora

**27.** Ni nini kinyume cha: Harufu nzuri imetamanisha mgeni.
A. Harufu mbaya imetamanisha mgeni.
B. Harufu nzuri imemtamanisha mwenyeji
C. Harufu mbaya imemtamausha mwenyeji
D. Harufu mbaya imemtausha mgeni

**28.** Chagua sentensi yenye hali ya kutendesha sahihi
A. Nani anamlilisha mtoto?
B. Usimwoleshe binti yako kwa babu
C. Mgonjwa amelazwa kwenye wadi
D. Tumesomezwa Kiswahili baada ya hesabu

**29.** Tegua kitendawili: Kutoa ni kuongeza
A. chimbo
B. mgodi
C. chakula
D. pesa

**30.** Neno la kuonyesha hisia za huruma au kuionea hali ya mtu huruma ni
A. Ashakum
B. Tafadhali
C. Samahani
D. Nasikitika

***Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali* 31 – 40**

Mzee mmoja mwanaume akiwa mbioni kasi sana alitokeza mashakani palipokuwa karibu, kandokando ya baraste huku amemfuata pofu aliyekuwa vilevile ameshika kasi ajabu kuokoa maisha yake. Huyo mnyama alipofika baraste alivuka kasi mithili ya umeme. Msasi naye maskini hakuhakikisha kama kwamba kulikuwa na magari. Alivuka mbio mbio kumfuata huyo pofu aliyekuwa ilsalamani. Alipofika katikati ya baraste kushtuka tu, gari lilikuwa safarini mbio likamgonga dafrao likamrusha juu kishaye akaanguka katikati ya barabara kwa kishindo pu! Dereva bila shaka alikuwa amejaribu awezavyo kumhepa lakini hakufua dafu! Matwana yenyewe ilisita hatua arubaini kutoka majeruhi alipokuwa. Mlio wa mshtusho wa ghafla ukifuatiwa na mkumbano baina ya mtu na gari hilo uliwagutusha watu waliokuwa karibu na wapita njia nao wakaja gwarideni kushuhudia jambo hilo la kutisha macho. Alipogundua kuwa bado alikuwa akipumua akaomba msaada wa kumbeba na kumwingiza ndani ya matwana huyo ambayo sasa ilikuwa imeegeshwa pande zote mbili za baraste. Pindi tu gari likang'oa nanga kasi likielekea hospitali moja mahususi, na mgonjwa wake mahututi, kilomita chache kilichotokea gari lenyewe.

---

**31.** Pofu alikuwa mbioni kuokoa __________
A. maisha ya wasafiri wa gari lile
B. maisha ya maskini msasi
C. maisha yake mwenyewe
D. maisha yake na mzee maskini

**32.** Aliyepigiwa dafrao ni
A. msasi na msasiwa
B. msasiwa na wasafiri
C. msasi na dereva
D. msasi peke yake

**33.** "Wakaja gwarideni..." Ina maana
A. walizunguka gari la dereva
B. walimzingira mgonjwa
C. waliizingira barabara
D. walimzingira yule pofu

**34.** Dereva aliomba msaada kwa
A. walio gwarideni
B. waliomo garini
C. walio kando kando karibu na barabara
D. wapita njia

**35.** Mzee huyo mwanaume alitaka
A. kupanda gari
B. kujiunga na wapita njia
C. kumwua pofu
D. kusalimika

**36.** Mnyama ________________.
A. alijiokoa kwa mbio
B. alinusurishwa na gari
C. waliokolewa na wapita njia
D. walinusurishwa na maskini mzee

**37.** Dereva hakufua dafu __________.
A. kumwua mzee
B. kumhepa pofu
C. kuliegesha gari
D. kumnusuru maskini msasi

**38.** Zahanati maalum hiyo ilikuwa
A. upande wa nyuma kutoka mahali pa ajali
B. upande wa mbele kulikotokea gari lile
C. upande ambao haukuelezwa katika hadithi
D. karibu na barabara

**39.** "Aliyekuwa usalamani" ina maana ya
A. aliyeuawa na mwindasi
B. aliyeponyoka
C. aliyevuka baraste
D. aliyesalimika na waliomo gari

**40.** Majeruhi ______________.
A. alikuwa dereva
B. walikuwa gwarideni
C. alikuwa mwindaji
D. alikuwa pofu

***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali* 41 – 50**

Mama nimekosa nini, mwanao kunikimbia,
Umeniachia nini, mwingine wa kunilea,
Nimebaki na huzuni, sina wa kumdekea,
kinda ningali mtini, sina mama kunilea,

Mimi na baba nyumbani, wenyewe twajipikia,
Baba anachaja kuni, nami mtoto nachochea,
Hukumbukia zamani, mama nakulilia,
Kinda ningali mtini, sina mana kunilea,

Niendapo kwa jirani, mchezo kujichezea,
Wenzangu huitwa ndani, nini nilichokosea,
Husononeka moyoni, nini nilichokosea,
Kinda ningali mtini, sina mana kunilea,

Umenibeba tumboni, miezi tisa kutimia,
Nimekua duniani, ghafla wanikimbia,
Umependa nini hasa, kuliko mimi radhia,
Kinda ningali mtini, sina mama kunilea,

---

**41.** Shairi hili ni la bahari gani?
A. Tathlitha
B. Takhmisa
C. Tarbia
D. Tasdisa

**42.** Taja mloto wa shairi uliyoisoma ubeti wa pili
A. wenzangu huitwa ndani, nini nilichokosea
B. baba anachanja kuni, nami mtoto nachochea
C. kuliko mimi radhia
D. umenibeba tumboni miezi tisa kutimia

**43.** Mshororo wa tatu ubeti wa pili una mizani ngapi?
A. 13 B. 14
C. 15 D. 16

**44.** Shairi hili lina beti ngapi?
A. 12 B. 256
C. 4 D. 64

**45.** Lawinji wa kutunga mashairi na nyimbo
A. mghani B. jagima
C. malenga D. manju

**46.** Ni vipi vina vya kati na vya mwisho vya ubeti wa tatu
A. ni, a B. ni, ea
C. ni, ni D. m, w

**47.** Kipande cha kwanza cha mshororo huitwa
A. utao B. ukwapi
C. mloto D. mwandamizi

**48.** Mshororo wa mwisho kwenye shairi hili tunaweza kuita majina haya ila
A. kibwagizo B. kituo
C. mkarara D. kiitikio

**49.** Mtunzi anasema, "Kinda ningali mtiini..." angusia nini?
A. Mama yake
B. Yeye binafsi
C. Ndiye mkubwa
D. Mimba yake

**50.** Kichwa bora kifaacho shairi hili ni
A. mama amenilea vyema
B. shukurani kwa mama
C. mama amenikimbia
D. nilivyomkosea mama